

## Kwa Pamoja!

Palikuwepona na Chifu mmoja aliyewaalika watu kwa sherehe kubwa. Watu walisafiri mbali na karibu kuhudhuria sherehe – walivalia mavazi yao nadhifu na walimletea Chifu zawadi. Chifu alifurahi sana kwa kuwa alitaka kuona ufalme wake na watu aliowaongoza.

Baada ya siku kadhaa alitambua kuwa watu wa kabila lake walilumbana. Walibishana na kutofautiana ju ya uzoefu na ubora wa kuhifadhi na kutunza mila na desturi au ni nani aliyeimba nyimbo nzuri zaidi. Watu wa kijiji kimoja waligombana, umoja na utangamano haukuwepo. Chifu alitambua kuwa watu hawakushirikiana tena.

Chifu alifadhaishwa na mambo haya kwa hivyo aliamua kuyashughulikia. Usiku moja aliamua kuwakusanya wazee wa Kijiji katika ukumbi mkubwa. Juu yao aliweka kisu kwa dari. Aliwaambia wazee kuwa yule atakayetwaa kisu hicho angekuwa Chifu. Aliahidi ufalme wake wote kwa yule atakayetwaa kisu.

Viongozi walishangaa na kwa tamaa wakaanza kupigana. Kila mmoja alijaribu kupanda lakini wakashindwa. Wengi wao walikuwa wanapigana na wakashau kutwaa kisu kabisa. Baada ya saa moja kila mmoja alichoka na kukata tamaa.

Kisha Chifu huyu mwenye busara akasema, “Kwa nini mnafikiri hakuna awezaye kufanya jambo hili? Haiwezekani kabisa, kwa sababu dari iko juu sana kuifikia.” Chifu alikusanya wanaume watano na kuwaelekeza wasimame ardhini, kisha wengine watatu walisimama juu ya mabega yao, wawili walisimama juu ya hao watatu. Wazee hawa walifanya kama walivyoelekezwa na Chifu, lakini bado hawakuweza kufikia kisu. Chifu mwenyewe alipanda juu ya wale wazee wawili na kutwaa kisu mwenyewe.

Iligharimu mchango wa kila mmoja kufikia na kutwaa kisu. Hata Chifu mwenyewe alihitaji msaada wa wengine ili afanikiwe.

Waefeso 2:19-22 inatuonyesha kuwa hili ndilo kanisa kwa kawaida: “Basi tangu sasa nyinyi si wageni wala wapitaji, bali nyinyi ni wenyeji pamoja na watakatifu, watu wa nyumbani mwake Mungu.”

### Zingatia!

Kwa nini msiwakaribishe baadhi ya watu kutoka makanisa mengine au vijiji vingine. Mkishiriki chakula, kuomba na kukaa pamoja kunatosha kutudhihirishia kuwa tuna nguvu zaidi tunapodumu katika umoja.


### Omba:

- 1) Kutakuwa na suluhu kwa ugomvi wowote ule.
- 2) Moyo wako utajaa huruma kwa ajili ya majirani zako.
- 3) Ufanisi utafikiwa tutakapofanya kazi pamoja.



"Nimetambua ya kwamba baadhi ya mambo yanayotuangamiza katika jamii zetu ni 'migogoro ya dini'. Lazima tuyaache hayo na tuweke mtazamo wetu kwa Kristo pekee."

**- Moses, Katima Mulilo, Namibia**



Somo hili limewezeshwa na “Maisha kupitia Jamii” somo linalopatikana ndani ya kitabu cha Panda: Mafunzo ya Msingi ya Vikundi Maisha.

Kinapatikana hapa:

**[dignityonline.org.uk/publications](https://dignityonline.org.uk/publications)**